



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Email- ded.itigidc@singida.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi  
01 Barabara ya Halmashauri  
S.L.P 70,  
43483 ITIGI - SINGIDA.

Unapojobu tafadhali taja:

Kumb. Na. HW/ITG/S1/22 VOL IV/54

03 Aprili, 2024.

Kwa wananchi wote

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imepokea kibali cha utekelezaji wa Ajira Mbadala katika mwaka wa fedha 2023/2024 chenye Kumb.Na. FA.228/613/01/A/052 cha tarehe 05 Februari, 2024 pamoja na Kibali cha Ajira Mbadala chenye kumb. Na. FA. 170/366/01”B”/122 cha tarehe 02 Agosti, 2023 Kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia Wananchi wote raia wa Tanzania wenyewe sifa, kuomba nafasi zilizoorodheshwa hapo chini.

**1. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 1)**

**Sifa za Mwombaji**

- Awe amefaulu kidato cha nne (IV)
- Leseni ya Daraja E au C<sub>1</sub> ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua Mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundis Stadi (VETA) au Chuo kinachotambuliwa na Serikali

## **Majukumu ya kazi ya Udereva**

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya Usalama wa gari
- Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- Kufanya usafi wa gari; na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

## **Mshahara**

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani TGS B/1 kwa Mwezi

## **2. MTENDAJI WA KIJINI DARAJA LA III – (NAFASI 1)**

### **Sifa za Mwombaji**

- Awe amefaulu kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI)
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (Cheti) ‘NTA Level 5” kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali katika fani zifuatazo:-
  - Utawala
  - Sheria
  - Elimu ya Jamii
  - Usimamizi wa Fedha
  - Maendeleo ya Jamii
  - Sayansi ya Jamii
  - Mipango na Maendeleo ya Vijijini

### **Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji**

- Katibu wa Kamati ya Kijiji
- Mtendaji wa Kamati ya Kijiji
- Mratibu wa Utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelizwa na Halmashauri katika Kijiji.
- Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Kijiji
- Msimamizi wa utekelezaji wa Sheria ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Kijiji

- Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama
- Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umasikini katika Kijiji
- Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

#### **Mshahara**

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani TGS B kwa mwezi

### **3. MASHARTI KWA UJUMLA**

- Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua Miaka Kumi na Nane (18) na usiozidi miaka Arobaini na Tano (45)
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatanishe na maelezo yao binafsi (C.V)
- Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya Taaluma, vyeti vya kidato cha (IV na VI), na picha moja ya rangi katika barua ya maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE
- "Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (FORM IV and FORM VI RESULT SLIPS)  
**HAVITAKUBALIWA**
- Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **17 Aprili, 2024** saa **9:30** Alasiri

Maombi yote yatumwe kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo:- <http://portal.ajira.go.tz/>. (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu ilioandikwa 'Recruitment Portal').

Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili  
**HAYATAFIKIRIWA**

Anuani ya barua ielekezwe kwa:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi,  
01 Barabara ya Halmashauri ,  
S.L.P 70,  
43483 ITIGI - SINGIDA.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:

  
Ayoub J. Kambi  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

**Nakala:** Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,  
S.L.P 2320,  
**DODOMA.**

- Mbao za Matangazo